# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO

**MKATABA**

**BAINA**

**YA**

**KATIBU MKUU WIZARA YA AFYA MAENDELEO YA JAMII JINSIA WAZEE NA WATOTO**

**S.L.P 128 DODOMA**

**NA**

**EMMANUEL KANONI**

**S.L.P 187 SUMBAWANGA**

**MKATABA WA UJENZI WA JENGO LA WAGONJWA MAHUTUTI KWENYE HOSPITALI YA RUFAA SUMBAWANGA**

Mkataba huu umetiwa saini leo tarehe .........29......... mwezi .........11.......... 2021

**BAINA YA**

**Katibu Mkuu Wizara Ya Afya Maendeleo Ya Jamii Jinsia Wazee Na Watoto**
, na ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama **"Mwajiri"** kwa upande mmoja.

**NA**

**M/S EMMANUEL KANONI, WA S.L.P 187, Sumbawanga** ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "**Fundi** "kwa upande wa pili tafsiri inayo jumuisha yeye, familia yake, wategemezi, warithi na yeyote mwenye maslahi kupitia Fundi huyo.

**KWAKUWA** Mwajiri anahitaji huduma ya kujengewa Jengo la Wagonjwa Mahututi kwenye Hospitali ya Mkoa ya Rufaa Sumbawanga katika mwaka wa fedha 2021/2022,

**NA KWA KUWA** Fundi ameonesha nia na uwezo (Willingness&Competence) wa kutoa huduma hiyo kwa Mwajiri.

**SASA BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIWA KAMA INAVYOONESHA HAPA CHINI:-**

**1. MUDA WA MKATABA.**

Mkataba huu utaanza kutumika siku atakapokabodhiwa eneo la ujenzi.
Mkataba huu utakuwa ni wa muda wa miezi minne toka tarehe ya kukabidhiwa eneo la Ujenzi

**2. NAMNA YA KUTOA HUDUMA.**

Fundi atatoa huduma husika baada ya kupokea Mkataba kutoka kwa Mwajiri.

**3. GHARAMA YA MKATABA.**

Gharama ya ufundi katika Mkataba huu wa Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa Mahututi itakuwa ni **Tshs. 36,470,000.00** (Milioni Thelathini na Sita, Laki Nne na Sabini tu)

## 4. MALIPO.

Mwajiri atakuwa na wajibu wa kumlipa Fundi mara baada ya huduma husika kutolewa na Fundi huyo ambapo Mwajiri kupitia Meneja wa Mradi atakagua kwanza kazi hiyo na kujiridhisha kabla hajaidhinisha malipo. Kwa njia ya maandishi Fundi atawajibika kuwasilisha maombi ya kuomba kulipwa kwa Mwajiri.

Fundi atalipwa 80% ya kila hatua ya malipo yake atakayoomba kulipwa, na 20% inayobaki atalipwa mwishoni baada ya kumaliza kazi yake ya ujenzi.

## 5. MASHARITI YA MKATABA.

- Mwajiri kupitia wataalamu wake pamoja na Meneja wa Mradi wanayo haki ya kutoa maelekezo kwa fundi kadri yatakavyohitajika ili kuboresha ujenzi na bila kuathiri makubaliano ya mkataba huu.
- Orodha ya kazi zitakazofanyika na gharama zake zilizoambatishwa ni sehemu halali ya Mkataba huuu
- Ni wajibu wa Fundi kutunza vifaa/vitendea kazi atakavyopatiwa na Mwajiri na endapo kutatokea uharibifu au upotevu wa vifaa hivyo, Fundi atawajibika kumlipa Mwajiri fidia inayoendana na vifaa vilivyopotea au kuharibiwa.
- Tozo ya ucheleweshaji kazi ya asilimia kumi (10%) itatozwa kwa fundi endapo atachelewa kumaliza kazi ndani ya muda wa Mkataba bila kuwepo na sababu za msingi.
- Lugha halali ya Mkataba huu ni Kiswahili.
- Fundi atafanya kazi kwa mujibu wa maelezo na mchanganuo wa kazi zake (kiambatisho)

## 6. UKIUKWAJI WA MASHARTI.

Endapo Fundi atashindwa kutimiza masharti ya mkataba huu ikiwa ni kuchelewesha au kutoa huduma ambayo haikidhi viwango na mahitaji ya Mwajiri, hatalipwa na Mwajiri hatahusika na hasara yoyote itakayosababishwa na uzembe wa Fundi.

**7. USULUHISHI WA MIGOGORO.**

Endapo kutatokea mgororo katika Mkataba huu utasuluhishwa kwa njia ya **majadiliano** na endapo itashindikana Sheria ya Utatuzi wa Migogoro Sura ya 291(**Arbitration Act Cp. 291**) itatumika.

**8. USITISHWAJI.**

Mkataba huu unaweza kusitishwa na yeyote kati ya **Mwajiri** au **Fundi** baada ya mmoja wao kutotimiza wajibu wake kama ilivyoainishwa hapo juu na usitishwaji huu utaambatana na notisi ya siku kumi na nne (14).

**9. UHALALI WA MKATABA HUU.**

Mkataba huu ni halali kwa mujibu wa Sheria za Tanzania. Na kwamba mkataba huu unatafsiriwa na kutawaliwa na Sheria za mikataba ya Tanzania na Sheria nyingine za Nchi na kwamba Mkataba huu umeandikwa kwa nakala tatu na kila nakala itatambuliwa kuwa ni nakala halisi ya Mkataba huu na kwamba hakuna upande wowote wa Mkataba huu utakaobadilisha Mkataba huu isipokuwa kwa idhini ya maandishi ya upande wa pili.

**KWA USHUHUDA** na **UTHIBITISHO**, Mkataba huu umewekwa saini na pande zote mbili **Mwajiri** na **Fundi** mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini: Gharama ya Mkataba huu wa Ujenzi **Tshs. 36,470,000.00** (Milioni Thelathini na Sita, Laki Nne na Sabini tu)

| **UPANDE WA MWAJIRI** | **SHAHIDI:** |
|---|---|
| **Jina:** DR ISMAIL MACHA | **Jina:** FRIDA I. HAVA |
| **Cheo:** MGANGA MFAWIDHI | **Cheo:** ADVOCATE |
| **Saini:** [signature] | **Saini:** [signature] |
| **Tarehe:** 29/11/20.. | **Tarehe:** 29/11/2021 |

MGANGA MFAWIDHI HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA SUMBAWANGA

FRIDA IDIFONCE HAVA Advocate, notary public & Commissioner for Oaths P.O.Box 128-SUMBAWANGA

| **UPANDE WA FUNDI :** | **SHAHIDI:** |
|---|---|
| **Jina:** EMANUEL P. KANONI | **Jina:** DIDAS E KATAPA |
| **Saini:** [signature] | **Saini:** [signature] |
| **Tarehe** 29/11/2021 | **Tarehe** 29/11/2021 |

# MPANGO KAZI WA MAFUNDI KWA KAZI YA UKARABATI WA JENGO WA WAGONJWA WA DHARULA (ICU) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA RUKWA (SRRH) MKOA WA RUKWA

NOVEMBA, 2021

# MPANGO KAZI WA MAFUNDI

## GHARAMA ZA UFUNDI KWA UKARABATI WA JENGO WA WAGONJWA WA DHARULA (ICU) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA RUKWA (SRRH)

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| A | **Msingi wa Jengo (Sub-structure)** | |
| | Kusafisha eneo | 150,000/= |
| | Kuseti jengo | 150,000/= |
| | Uchimbaji wa msingi | 250,000/= |
| | Kufukia | 100,000/= |
| | | |
| | **Usukaji wa Nondo katika;** | |
| | Ground beams" | 250,000/= |
| | | |
| | **Kufunga mbao** | |
| | Pembezoni mwa jamvi | 200,000/= |
| | Pembezoni mwa Nguzo mlalo 'Ground beams" | 200,000/= |
| | Kuondoa mbao | 50,000/= |
| | | |
| | **Kumwaga zege** | |
| | Chini kwenye msingi | 200,000/= |
| | kwenye jamvi pamoja na "beams" | 1,200,000/= |
| | Ujenzi wa tofali za msingi | 1,000,000/= |
| | Kuondoa mbao | 50,000/= |
| | | |
| | **Mawe** | |
| | Upangaji wa mawe na utandazaji wa DPM | 1,920,000/= |
| | Umwagiliaji wa maji | 700,000/= |
| | **Jumla ndogo msingi wa jengo** | 6,370,000/= |
| | | |
| B. | **Kunyanyua jengo (Super-structure)** | |
| | Ujenzi wa tofali za kuta na uwekaji DPC | 2,500,000/= |
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| | **Kufunga mbao katika:** | |
| | Nguzo mlalo 'Ground beams" | 350,000/= |
| | **Kusuka nondo katika:** | |
| | Nguzo mlalo | 450,000/= |
| | | |
| | **Kumwaga zege katika:** | |
| | Nguzo mlalo | 500,000/= |
| | Umwagiliaji wa maji | 100,000/= |
| | **Jumla ndogo Kunyanyua jengo (Super-structure)** | 3,900,000/= |

**GHARAMA ZA UFUNDI KWA UKARABATI WA JENGO WA WAGONJWA WA DHARULA (ICU) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA RUKWA (SRRH)**

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| C. | **Kuezeka (Roof structure and covering)** | |
| | Kuezeka | 1,800,000/= |
| | **Jumla ndogo Kuezeka** | 1,800,000/= |
| D. | **Milango** | |
| | Kufitisha fremu za milango | 300,000/= |
| | Kufitisha shata za milango pamoja na vitasa | 300,000/= |
| | Upakaji wa Varnishi katika milango na fremu | 200,000/= |
| | Uwekaji wa vioo katika venti za milango | 200,000/= |
| | **Jumla ndogo Milango** | 1,000,000/= |
| E. | **Madirisha** | |
| | Utengenezji wa dirisha za Aluminium | |
| | **Jumla ndogo Madirisha** | — |
| F. | **Umaliziaji (Finishing)** | |
| | Upigaji wa lipu pamoja na kutengeneza koplo: | |
| | Nje ya jengo | 1,500,000/= |

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| | Ndani ya jengo | 1,500,000/= |
| | Sakafu | |
| | Uwekaji wa sakafu ya kupokea vigae (beds) na Apoxy paint | 1,500,000/= |
| | Uwekaji wa vigae pamoja na grauti katika sakafu (floor tiles) | 1,500,000/= |
| | Uwekaji wa Apoxy paint- | 2,500,000/= |
| | Dali: | |
| | Ufungaji wa mbao za dali (Brandering) | 1,000,000/= |
| | Uwekaji wa dali na mikanda ya gypsum | 1 800,000/= |
| | Uwekaji wa vigae katika kuta na upakaji grout | 650,000/= |
| | Jumla ndogo umaliziaji(finishing) | 11,950,000/= |
| G. | Rangi na Mapambo (Painting & Decoration) | |
| | | |
| | Kupaka rangi mikono mitatu pamoja na skimming katika: | |
| | Kuta za nje | 1,600,000/= |
| | Kuta za ndani | 1,600,000/= |
| | Dali | 800.000 |
| | Kupaka rangi mikono mitatu katika: | |
| | Msingi wa nyumba | |
| | Fisherboard na Roof Vents | 800,000/ |
| | | |
| | Jumla ndogo Rangi na mapambo | 4,800,000/= |
| | | |
| H. | Umeme (Electrical installation) | |
| | Usukaji wa umeme awamu ya kwanza - Conduit na Box | 1,000,000/= |
| | Usukaji wa umeme awamu ya pili (2nd fix)-fittings | 2,500,000 |
| | Jumla ndogo Umeme | 3500,000/= |

GHARAMA ZA UFUNDI KWA UKARABATI WA JENGO WA WAGONJWA WA DHARULA (ICU) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA RUKWA (SRRH)

| Na. | AINA YA KAZI | BEI YA UFUNDI - TZS |
|---|---|---|
| | | |

| | | |
|---|---|---|
| I. | **Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system)** | |
| | Ufungaji bomba awamu ya kwanza (Kuchimbia bomba) | 500,000/= |
| | Ufungaji bomba awamu ya pili (2nd fix) -fittings | 1,500,000 |
| | Ufungaji wa Mifumo ya maji ya mvua | — |
| | Kuunganisha bomba za maji taka katika mashimo na chemba | 500,000/= |
| | **Jumla ndogo Mifumo ya maji safi na taka** | 2,500,000/= |
| J. | **Manholes** | |
| | Uchimbaji Chemba 'Manholes" | 150,000/= |
| | Kujenga tofari za chemba | 500,000/= |
| | **Jumla ndogo Ujenzi wa Septic tank & Manholes** | 650,000/= |

**GHARAMA ZA UFUNDI KWA UKARABATI WA JENGO WA WAGONJWA WA DHARULA (ICU) HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA RUKWA (SRRH)**

| | MAJUMUISHO (SUMMARY) | TZS |
|---|---|---|
| A. | Msingi wa Jengo (Sub-structure) | 6,370,000/= |
| B. | Kunyanyua jengo (Super-structure) | 3,900,000 |
| C. | Kuezeka (Roof structure and covering) | 1,800,000 |
| D. | Milango | 1,000,000 |
| E. | Madirisha | — |
| F. | Umaliziaji (Finishing) | 11,950,000/= |
| G. | Rangi na Mapambo (Painting & Decoration) | 4,800,000/= |
| H. | Umeme (Electrical installation) | 3,500,000 |
| I. | Mifumo ya maji safi na taka (Water Supply and Sewage system) | 2,500,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| J. | Septic tank, Soakwaypits & Manholes | 650,000/= |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | | |
| | **JUMLA KUU** | 36,470,000/= |

**ANGALIZO:**

Fundi anatakiwa kujaza hii fomu kwa kupitia michoro ya jengo husika pamoja na kupata maelekezo ya kina kutoka kwa Wataalamu wasimamizi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)